OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI
SHULE YA SEKONDARI NDOLWA
S.L.P 262
HANDENI-TANGA.

Kumb NO.NSS/ADM/FI/2021/........

JINA LA MWANAFUNZI ..........................................................................

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDOLWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ndolwa ambayo ipo kijiji cha Mzundu kata ya ndolwa. Hongera sana. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 (Mzazi unatakiwa umlete mwanao). Kikao cha kwanza cha wazazi kitafanyika tarehe 11/01/2021 saa mbili kamili asubuhi (08:00 asubuhi). Mzazi unatakiwa kuja na mwanao kwenye kikao hicho. Mzazi ambaye hatafika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

(i) Sare ya Shule.

Sare ya shule ni suruali mbili (2) za kaki kwa wavulana na sketi mbili (2) za kaki kwa wasichana, mashati meupe mawili (2) ya mikono mifupi kwa wavulana na wasichana.

NB: Wasichana wanaoweza kushona hijabu washone za rangi nyeupe.Wavulana washone suruali pana isiwe ya kubana (inchi 18 upana), mkanda mweusi kwa wavulana, viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba kwa wasichana na wavulana, soksi nyeupe ndefu kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

**Sare ya michezo:**

- Bukta ya bluu kwa wavulana na **track suit** ya bluu kwa wasichana, T-shirt ya bluu kwa wote, raba na soksi.

**(ii) Vifaa vya darasani**

(a) Aje na daftari 10 kubwa.
(b) Kamusi ya kiingereza.
(c) Kalamu na penseli pamoja na rula.
(d) Mkebe wa vifaaa vya hisabati (mathematical set).
(e) Karatasi za kutosha kwa ajili ya mazoezi yake ya darasani.

Mambo mengine muhimu

- Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya serikali. Fomu itakabidhibiwa kwa mkuu shule.
- Bima ya Afya (CHF) ni muhimu sana kwa mwanao hakikisha anayo.
- Fomu ya tamko la mzazi. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule.
- Fomu ya sheria na kanuni muhimu za shule hii ambayo mwanafunzi anatakiwa kuwa nayo muda wote.
- Shule ina hostel kwa wasichana nafasi ni chache.
- Mwisho Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na utekeleze kikamilifu

Karibu sana Ndolwa sekondari

Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Ndolwa
S.L.P. 262 Handeni

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI NDOLWA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Wanafunzi wote wa shule ya Ndolwa Sekondari wanapaswa kuzingatia na kufuata sheria za shule kwa mujibu wa sheria za Elimu Na 25. ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana na elimu nchini kama ifuatavyo;

1. Wanafunzi lazima waheshimiane wenyewe kwa wenyewe na wawaheshimu walimu wao, watumishi wengine wa shule na watu wengine, wasimame apitapo mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri.

Wanafunzi lazima wathamini na kuheshimu kazi za mikono na waclewe ni sehemu ya mafunzo yao ya maisha. Kidato cha kwanza kila mwaka watachukua jukumu lote la usafi hivyo ni wajibu wake kujituma bila kusukumwa.

Ni marufuku kabisa mwanafunzi

i. Kutumia lugha mbaya kama matusi shuleni au nje ya shule.
ii. Kunyoa mitindo ya kipara bila kuwa na msiba au kunyoa panki.
iii. Kupiga makelele darasani au katika mikutano au mikusanyiko mingine.
iv. Kuvaa sare pamoja na nguo ambazo siyo sare ya shule. Pia kuvaa hereni, bangili, vibanio na mapambo mengineyo
v. Kufuga kucha ndefu na kupaka kucha rangi au kujichora mwilini kufuga ndevu na nywele ndefu
vi. Kuwa mchafu wa mwili na mavazi. .
vii. Kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu
Viii. Kutembelea baa, vilabu vya pombe, majumba ya starehe na majumba ya kufikia wageni.
ix. Kuwa mvivu na legelege katika shughuli zote za shule ndani na nje ya darasa ‘ Ahudhurie mafunzo yote ya ukakamavu hapa shuleni’.
x. Kuvuta sigara, kuvuta bangi, kinywa pombe, kutumia madawa ya kulevya na uasharati.

Kila mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na vya nje ya darasa na kushiriki kikamilifu bila kuchelewa au kujishauri. Kila mwanafunzi lazima aheshimu wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na fedha
za Taifa. Kila mwanafunzi anawajibika kutunza mali za shule na zake binafsi. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na begi la shule kwa ajili ya kubebea vifaa vya shuleni marufuku kukunja daftari au kitabu na kuweka mfukoni.

Mwanafunzi atafukuzwa shule kwa kufanya makosa yafuatayo:
(a) Wizi
(b) Uasherati, ubakaji na ushoga.
(c) Utumiaji wa madawa ya kulevya kwa mfano kuvuta sigara, bangi, n.k.
(d) Kupigana, kupiga au kutishia kupiga.
(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya umma.
(f) Kuoa au kuolewa.
(g) Kupata mimba au kutoa mimba au kusababisha mimba nje au ndani ya shule.
(h) Kugoma, kuchochea mgomo au kuongoza mgomo.
(i) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(j) Kutohudhuria shule muda mrefu bila ya sababu za msingi
(k) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

**Kila mwanafunzi anapaswa kufahamu sheria za shule na kuzifuata kikamilifu.**

KIAMBATISHO “A”
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SECONDARI YA KUTWA NDOLWA
FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA

SEHEMU A
HABARI ZA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi)

1. Jina kamili ..................................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ________________ Dini _____________________
3. Mahali ulipozaliwa mji/kijiji ______________________________________________
4. Mahali unapoishi sasa ____________________________________________________
5. Anuani _________________________________________________________________
6. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ________________________________________

NAKUBALI NAFASI (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi ________________________________________________ ambaye maelezo yangu ni hayo hapo juu nimesoma maagizo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Ndolwa na ninakubali kutimiza masharti yote na kutii sheria ya shule.
Nakiri kwamba fomu hii nimejaza nikiwa na akili timamu bila kushurutishwa na mtu yeyote. Sina kipingamizi chochote.

Sahihi ya Mwanafunzi _______________________________

Tarehe ______________________________

SEHEMU “B”
HABARI ZA MZAZI AU MLEZI (Ijazwe na Mzazi)

1. Jina kamili _______________________________________________
2. Mzazi/mlezi _______________________________________________
3. Kazi _______________________________________________________
4. Mahali unapoishi __________________________________________
5. Anuani ____________________________________________________
6. Namba ya simu ____________________________________________
7. Sahihi ____________________________________________________
8. Tarehe ____________________________________________________

Nimesoma maagizo yote na kuelewa na nitajitahidi kutekeleza na kushiriki katika malezi ipasavyo bila kushawishiwa na mtu yeyote. Nikikiuka hatua kali zichukuliwe dhidi yangu na mwanangu.

APPENDIX "C"

HANDENI DISTRICT COUNCIL
NDOLWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 262 HANDENI

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by Medical Officer in respect to form I/V

Pupil's full name ..........................................................................................................

Age ...............................................................................................................................

Blood count (Red and White) .......................................................................................

..........................................................................................................

Stool ...............................................................................................................................

Urinalysis .......................................................................................................................

Syphilis test ....................................................................................................................

T.B test ...........................................................................................................................

Ears ................................................................................................................................

Chest ..............................................................................................................................

Spleen ............................................................................................................................

Abdomen ........................................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION: - E.g. Physical defects or Impairments, infection, chronic or family diseases, etc.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

I certify the above is fit/unfit for admission into a secondary school

Designation ...................................................................................................................

Station ...........................................................................................................................

Date ...............................................................................................................................

Official stamp